MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY

# UFALME WA MUNGU

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha  UFALME WA MUNGU. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

UFALME WA MUNGU

1.Ufalme wa Mungu ni nini ?…………………………….

2. Ishara za Ufalme wa Mungu…………………………..

3. Matunda ya ufalme wa Mungu……………………….

4. Haki za Ufalme wa Mungu……………………………

5. Unafananaje huo Ufalme wa Mungu?…………….

6. Unaukaribishaje Ufalme wa Mungu……………….

7. Ufalme wa Mungu ulikuja lini?………………………

8.Kodi ktk ufalme wa Mungu…………………………….

9.Ufalme wa mungu ni roho mtakatifu………………..

10.Kuokoka…………………………………………………….

11. Mwisho……………………………………………………

## 1. UFALME WA MUNGU NI NINI?

Ufalme wa Mungu ni utawala unaotawala mbinguni kwa 100% na duniani kwa kanisa la Yesu la waliokoka.Una mamlaka na nguvu kupita falme na mamlaka za giza,wakuu wa giza na pepo au majeshi ya pepo ktk ulimwengu wa rohot tena una uadui nazo zikukutanapo vita hupiganwa.

Mungu ndiye Mfalme ktk ufalme wa mbinguni . Kama mfame anatawala malaika na viumbe vya mbinguni 100% kwa roho yake takatifu iliyo ndani ya malaika na viumbe vya mbinguni.

Pia kama mfalme anatawala wanadamu waliokoka kwa njia ya roho mtakatifu aliye ndani yao.

Yesu pia ni Mfalme wa wayahudi lakini pia ni mfalme wa waliokoka mungu amempa kanisa na watakatifu walio mbinguni sehemu ya ufalme wake mungu atawale kwa sababu ni mwanaye pekee ampendaye aupendezaye moyo wa mungu.

**Mathayo 21:5**

**“Mwambieni binti Sayuni Tazama, mfalme wako anakuja kwako, Mpole, naye amepanda punda, Na mwana-punda, mtoto wa punda. “**

**1Timotheo 6.13—14**

**“Nakuagiza mbele za Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na mbele za Kristo Yesu, aliyeyaungama maungamo mazuri yale mbele ya Pontio Pilato, kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo; “**

Maandiko mtakatifu yanathibitisha Yesu ni Mfalme wa Wayahudi au Israeli kipindi hicho lilikuwa taifa la Mungu kwa sasa waliokoka.

# 2.ISHARA ZA UFALME

Utafahamu vipi kuwa ufalme wa Mungu upo ndani yako au ktk kanisa la waliokoka unapoabudu ee mtu wa kimataifa uliyeokoka? Zipo ishara zinazotabulisha ufalme u ndani yako au ktk kanisa unapoabudu nazo ni :=>

- kusema kwa lugha mpya;
- Unabii (Mwonaji)
- Uponyaji
- kutoa pepo;
- Karama ya Imani
- wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya.
- Miujiza
- Matendo ya Miujiza
- Kupambanua roho
- Tafsiri za lugha (za Malaika na za wanadamu)
- Neno la maarifa
- Neno la Hekima

Ufalme wa mungu kuwa ndani yako ni roho mtakatifu kuwa ndani yako huyo umempata njia ya kuokoka ee mtu wa kimataifa uliyeokoka.Na ufalme wa mungu kutawala ndani ni huyo msaidizi roho mtakatifu aliye ndani yako kukuongoza ktk kweli.

Palipo Roho mtakatifu au nguvu za mungu zikitenda kazi za kuokoka, uponyaji miujiza n.k ufalme wa mungu upo hapo.

Ishara nyingi zilizoorodheshwa hapo juu ni karama za Roho mtakatifu ukiziona ufahamu ufalme wa Mungu u ndani yako.

Mabadiliko unayohisi ndani yako ee mtu wa kimataifa uliyeokoka yatokana karama alizokupa Roho mtakatifu.

## 3. MATUNDA YA UFALME WA MUNGU

Matunda ya ufalme wa Mungu ni matokeo ya ufalme kukua ndani yako au ktk wokovu wako (Maisha mpya baada ya kuokoka kwa kutii neno la Yesu na kutendewa mema kama uponyaji, miujiza, baraka, kutolewa pepo na nguza za giza) ee mtu uliyeokoka wa kimataifa

**Warumi 14.17**

**" Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu."**

**Wagalatia 5.22 – 23**

**"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. "**

Tunda la roho ni badiliko linaloanzia ndani yako mpaka kwenye matendo ya maisha yako mpya kwa kutii mafundisho,maagizo na nabii za Yesu kwa kuhudumiwa na watumishi waliotumwa Yesu Kama Mitume,Waalimu wa kanisa,Manabii ,waandishi na Wachungaji .

Tunda la roho ni matokeo ya kupokea na Roho mtakatifu na kumpa nafasi ya kukuongoza ktk kweli na yeye ndio huo ufalme wa mungu kumpokea ni sawa kupokea ufalme wa mungu.

Matunda ya ufalme wa mungu yaani roho mtakatifu ni Amani,Haki, Furaha,Upendo,Uvumilivu,utu wema,Fadhili,Uaminifu,upole na kiasi.Jichunguze yapi unayo na yapi huna ktk wokovu wako? Mwombe baba wa mbinguni kwa roho mtakatifu aliye ndani yako akuze ufalme wake ndani yako na kukupa yale ambayo huna. Maandiko yanasema juu ya mambo hayo hakuna sheria yaani Ukitafuta hayo ukayapata huwezi kutenda dhambi ndipo wokovu unaheshimika mbele za mungu na watu Mungu ni rahisi kukutumia kama Yesu.

## 4. HAKI ZA UFALME ZA MUNGU

**Imeandikwa ktk Math 6:33**

**"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa. "** Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka wewe ni mwenyeji ktk ufalme wa mungu. Zipo haki unatakiwa kutendewa na Baba wa mbinguni ktk ufalme wake kama mwana unatakiwa kuzifahamu . Baadhi ya haki hizo ni kama;

- Chakula na Mavazi — **Mathayo 6:31**
- Elimu ya wokovu — **Mathayo 28:20**
- Kulindwa — **Yohane 17:12**
- Kubatizwa kwa maji mengi kama Yesu Ubatizo wa Toba unafatiwa na Roho mtakatifu (**Mathayo 3:15**)
- kuomba na kupewa (**Mathayo 7:7** )
- Kupewa uzima tele (**Yohane 10:10**)
- Kupewa roho mtakatifu akuongoze ktk kweli
- Kufanya kazi za Mungu kama kutoa pepo au kuponya wagonjwa **(Marko 16:14-18)**

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka hizo ni baadhi ya haki za ufalme wa mungu unapaswa kuzitafuta mbele za Baba wa mbinguni ktk ufalme wake ili akupe kwa maombi na kutii neno la Yesu. Ktk injili **(Mathayo,Yohane,Marko,Luka).**Elimu ya wokovu,ubatizo na roho mtakatifu ni haki zako za muhimu sana ktk kanisa ulilochagua kwenda kumwabudu hasa waliokokoka ee mtu wa kimataifa uliyeokoka hivyo unapaswa kuziulizia utaratibu kwa watumishi wa kanisa kama zipo ili ufuate utaratibu ili uzipate haki hizo za ufalme wa mungu.

## 5. UNAFANANAJE HUO UFALME WA MUNGU?

**Mathayo:13:31-32**

**"Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na punje ya haradali, aliyoitwaa mtu akaipanda katika shamba lake;**

**nayo ni ndogo kuliko mbegu zote; lakini ikiisha kumea, huwa kubwa kuliko mboga zote, ikawa mti, hata nyuni wa angani huja na kukaa katika matawi yake."**

Mfano wa haradali wa ufalme wa mungu una maana gani kwako ee mtu wa kimataifa uliyeokoka. Ulipookoka uliupokea ufalme wa mungu ndio huyo Roho mtakatifu aliye ndani yako kama msaidizi unafafana na punji ya haradali.Kila siku utoe masaa 3 kumwombe ukasaidie ktk mambo yale aliyokuamuru Yesu kama kukuongoza ktk ukweli yaani kukuongoza usitende dhambi,mshuhudie Yesu ktk wokovu wako huyo roho mtakatifu akutumia kufanya za yesu kama kuponya pia atakutendea mema ya Yesu kama miujiza, kukubariki, kukuponya,Kukufundisha biblia habari za yesu zilizo ktk injili ya Yesu kama Kitabu cha Marko ktk biblia,kukumbusha maagizo yatokayo ktk biblia. Usaidizi huo ukikua ndani yako ufahamu ufalme wa mungu unakua ndani yako mfano ukifika hatua ya kushuhudiwa na mungu huna dhambi na wanadamu pia kutokana Kumtii roho mtakatifu akiongoza ktk kweli yaani kukuonga usitende dhambi unaitwa mwana wa mungu na umekua kule ktk ufalme wa mungu mtu mzima si mtoto tena Hivyo hupendwa na mungu na kutumiwa naye kama Yesu.Kadri unavyompa roho mtakatifu nafasi moyo ndivyo ufalme wa mungu unavyokua ktk wokovu wako.Tunda la Roho mtakatifu kama upendo, Amani, Furaha, upole, kiasi,uvumilivu na haki yataoneka ktk wokovu utafanya wengine waokoke utazalia Bwana Yesu matunda ya kudumu ndio hao waliokoka kupitia wewe.

## 6 . UNAFANANAJE HUO UFALME WA MUNGU?

**Mathayo 13.24 — 30**

"Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake; "

" Lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake.Baadaye majani ya ngano yalipomea na kuzaa, yakaonekana na magugu. Watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? Limepata wapi basi magugu? Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka twende tukayakusanye? Akasema, La; msije mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo.

Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu. "

**Mathayo 13.36—39**

Kisha Yesu akawaaga makutano, akaingia nyumbani; wanafunzi wake wakamwendea, wakasema, Tufafanulie mfano wa magugu ya kondeni. Akajibu, akasema, Azipandaye zile mbegu njema ni Mwana wa Adamu; lile konde ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu; yule adui aliyeyapanda ni Ibilisi; mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ktk mfano huu umefanana na mbegu njema wewe ni mwana wa ufalme uwe hodari wa kutenda yaliyo haki ktk ufame wa mungu hilo litawezekana kwa kujizoeza kuongozwa ktk kweli na Roho mtakatifu na kutii neno la kristo.Yeye atakufanya utende haki.

7. UNAFANANAJE HUO UFALME WA MUNGU?

**Mathayo 13:44**

**"Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina iliyositirika katika shamba; ambayo mtu alipoiona, aliificha; na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalinunua shamba lile. "**

Ee mtu wa kimataifa uliyokoka au bado wewe uliye bado unapaswa kuokoka yaani kutubu,kubatizwa kama Yesu na kujazwa roho mtakatifu huyo ngiye ufalme wa mungu.Lakini wewe uliyeokoka ufalme wa mungu u ndani yako.

Ktk maandiko hayo neno "hazina" yale yote unayohitaji ktk maisha yako yalimo mema na yenye uzima yanapatikana kwa njia ya Yesu tena akikupa yana kufanya baada maisha yako ya wokovu ktk dunia hii unafika mbinguni kwa Baba yake Yesu.

Hazina yaani pengine Mali,Furaha,Mke mzuri,Pesa, Upendo, uta-Baraka, ukwasi,Nguvu .Mungu labda unatafuta mungu.

**Mathayo 13:33**

**"Akawaambia mfano mwingine; Ufalme wa mbinguni umefanana na chachu aliyoitwaa mwanamke, akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga, hata ukachachwa wote pia. "**Ufalme wa mungu ni huyo robo mtakatifu ni kama chachu ukimpa nafasi moyoni mwako atawala maisha mapya ya ufufuo wa Yesu yaani wokovu na kukufanya uzae matunda ya kudumu uwahubiri/uwashudie watu wa kimataifa wenye dbambi waokoke na kudumu ktk imani ya wokovu ambayo ni matokeo ya kumwamini Yesu kama wewe ulivyookoka kudumu ktk imani ya Yesu.Mbali na Yesu kukutumia ktk kuhubiri/kushuhudia wenye dhambi wafikie maamuzi ya kuokoka na kuokoka pia ukitii Roho mtakatifu Yesu akubadilishe matendo ya kila siku yawe na Kunda la Roho kama kiasi,furaha,Upendo na Amani hivyo huwezi kutenda

## 8. . UNAFANANAJE HUO UFALME WA MUNGU?

Mathayo 13:45—50

**"Tena ufalme wa mbinguni umefanana na mfanya biashara, mwenye kutafuta lulu nzuri;**

**naye alipoona lulu moja ya thamani kubwa, alikwenda akauza alivyo navyo vyote, akainunua.**

Lulu ni Madini ya thamani Kuokoka ni kama Lulu Ee mtu wa kimataifa mwenye dhambi ulikuwa siku nyingi unatafuta uokoke neema ilikuwa hajakufikia mwenye dhambi wewe ni kama huyo mfanyabiashara leo utafakaripo Kitabu hiki fanya maamuzi ya kuokoka na uokoke ununue hiyo kuokoka ni kwa thamani kupita lulu kwenye maisha yako iko sala ya kuokokamwisho wa kitabu unaweza kuifuatisha ndipo utakaponunua hiyo lulu vyote Vyema vyenye uzima atakulipa kwa wakati wake avifamuvyo Yesu atakulipa kwa wakati wake ukimtii roho mtakatifu na sauti yake Bwana Yesu.

Mathayo 13:47—51

**" Tena ufalme wa mbinguni umefanana na juya, lililotupwa baharini, likakusanya samaki wa kila namna;**

**hata lilipojaa, walilivuta pwani; wakaketi, wakakusanya walio wema vyomboni, bali walio wabaya wakawatupa. Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia; malaika watatokea, watawatenga waovu mbali na wenye haki, na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. "**

Mfano maana ni hii juya kutupwa ktk bahari unakutana mtumishi wa Yesu akikuhubiri au kukushudia ee mtu wa kimataifa mwenye dhambi uokoke ukiokoka jina la Yesu unafanana walio wema mliokoka tayari ndivyo ulivyo pia.

## 9. . UNAFANANAJE HUO UFALME WA MUNGU?

**Mathayo 18 : 23— 35**

“Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. Alipoanza kuifanya, aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi. Naye alipokosa cha kulipa, bwana wake akaamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo, ikalipwe ile deni. Basi yule mtumwa akaanguka, akamsujudia akisema, Bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia. Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe ile deni. Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia akamkamata,akamshika koo,akisema Nilipe uwiwacho. Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake, akamsihi, akisema, Nivumilie, nami nitakulipa yote pia. Lakini hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni. Basi wajoli wake walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka. Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi; nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe? Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote.

Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake.

Ndani ya ufalme wa mungu jifunze kusamehe wakukosea hata walioka usikae na uchungu moyoni usije ukagua ugonjwa kama B,P unapomkosea mwingine jifunze kutubu na kuomba msamaha.

## 11.. UNAFANANAJE HUO UFALME WA MUNGU?

**Luk 15:11 –22**

Akasema, Mtu mmoja alikuwa na wana wawili; yule mdogo akamwambia babaye, Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia. Akawagawia vitu vyake. Hata baada ya siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote, akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali zake huko kwa maisha ya uasherati. Alipokuwa amekwisha tumia vyote, njaa kuu iliingia nchi ile, yeye naye akaanza kuhitaji. Akaenda akashikamana na mwenyeji mmoja wa nchi ile; naye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe. Akawa akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu.

Alipozingatia moyoni mwake, alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako. Akaondoka, akaenda kwa babaye. Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana. Yule mwana akamwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena. Lakini baba aliwaambia watumwa wake, Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi; kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia. Basi, yule mwanawe mkubwa alikuwako shamba na alipokuwa akija na kuikaribia nyumba, alisikia sauti ya nyimbo na machezo. Akaita mtumishi mmoja, akamwuliza, Mambo haya, maana yake nini? Akamwambia, Ndugu yako amekuja, na baba yako amemchinja ndama aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu mzima. Akakasirika, akakataa kuingia ndani. Basi babaye alitoka nje, akamsihi. Ukitenda dhambi jifunze kutubu.

## 10. UNAUKARIBISHAJE UFALME WA MUNGU

Unaukaribishaje ufalme wa mungu ktk maisha yako kwa kuokoka yaani kutubu kubatizwa kama Yesu na kujazwa roho mtakatifu.

**Matendo ya Mitume** 2 : 1-47

2.1 Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja.

2.2 Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.

2.3 Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto ulio-wakalia kila mmoja wao.

2.4 Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.

2.5 Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu.

2.6 Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe.

2.7 Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya?

2.8 Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?

2.37 Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?

2.38 Petro akawaambia, **Tubuni mkabatizwe** kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha **Roho Mtakatifu.**Ktk matendo 2 mitume waliupokea ufalme wa mungu kwa mara kwanza

## 11. UFALME WA MUNGU ULIKUJA LINI?

Ufalme wa mungu ulikuja kwa wote wamwaminio mungu Baba yake Yesu muumbaji siku ya pentecoste siku chache baaada ya kufufuka kwake na kupaa mbinguni Bwana wetu Yesu **Matendo 2** Hiyo ndiyo siku Roho mtakatifu alishuka kwa mitume na wafuasi ambao nao waliwahubiri injili wenye dhambi waliokumbali Yesu ni Bwana na Mwokozi na kubatizwa walipewa Roho mtakatifu pia na kuwa kanisa tofauti na Agano la kale Roho mtakatifu walipewa wachache sana kama manabii na wafalme wa Israeli.

Ufalme wa Mungu ni Roho mtakatifu Kwa ni nini? Yatafakari haya maandiko:

**Marko 9:1**

**"Akawaambia, Amin, nawaambia, Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu. "**

Ktk maandiko haya Yesu alisema na mitume na wafuasi wake ambao wasingelikufa yaani kuonja mauti kabla kupewa roho mtakatifu na Mungu awe Msaidizi kwao ndio Pentecoste. Waliishi tangu siku waliposema neno hilo hadi Yesu alipofufuka na kupaa mbinguni.Siku chache baadaye walipewa roho mtakatifu.

**Matendo 2:1—4**

**"Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja.**

**Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho" .**

Ufalme Mungu unaukarishaje ktk maisha yako? Kwa Kuokoka kwa jina la Yesu yaani kutubu,Kubatizwa na kujazwa Roho mtakatifu Kwa jina La Yesu.

## 12. KODI KTK UFALME WA MUNGU

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka Lazima ulipe zaka au fungu la kumi ni sadaka ktk ufalme wa Mungu iliyo mfano wa kodi ktk nchi za dunia hii unayotoka ktk kazi za mikono. Watu hutoa au hukatwa kodi ktk mishahara,biashara au ujira wao kwa maendeleo ya nchi ndivyo ilivyo ktk ufalme wa Mungu.

**Malaki 3:10 –11**

**“ Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. “**

Zaka au fungu la kumi kama unakumbuka hesabu ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ni 1/10 au 10% ya mshahara,ujira wako wa kazini na 1/10 au 10% ya mapato uyapatayo ktk sehemu ulizowekeza kama unazo mfano  mgawaha wako , kampuni ya nguo,hoteli,maduka n.k

Utoapo fungu la kumi tarajia baraka kutoka Kwa Mungu Baba yake Yesu ndiye mfalme mkuu ktk ufalme wa mungu.Baraka itakuja ktk kazi unayofanya au sehemu ulizowekeza. Wewe Kama unapenda Baraka Ee mtu wa kimaitaifa Tafuta kanisa la waliokoka  mwanzilishi wao wao ana huduma ya kinabii mbali na zingine ukae tuli chini upako wa kinabii unaoendana Baraka.

Wewe kama mwenye ktk ufalme wa mungu uwe shahidi wa Barakaa ktk kazi za mikono yako ziinuazo mapato yako kuliko kwanza yaani ka-bla hujaokoka.

## 13.UFALME WA MUNGU NI ROHO MTAKATIFU

Ufahamu neno hilo ni kweli wenyeji wote wa mbinguni wana Roho mtakatifu kama msaidizi ktk wokovu wao. Na wewe uliyeokoka mtu wa kimataifa u mwenyeji kule nyumbani mbinguni kwa Baba yake Yesu.Wewe ni mwanaye kama alivyo Yesu yeye ni mwana wa kwanza Kwa Baba wa mbinguni yaani Mungu.Huu ndio msaada autoa roho mtakatifu ndani yako kutoka ktk ufalme wa Mungu au Yesu.

- Kukumbusha yote yatokayo kwa Yesu
- Kukufundisha yote yatokayo kwa Yesu
- Kumshuhudia Yesu ndani yako na ktk wokovu
- Kuwahakikishia ulimwengu juu dhambi,haki na hukumu
- Kukuongoza ktk kweli
- Kukushauri ushauri utokao kwa Yesu
- Kukupasha habari juu ya mambo ya baadaye.

**Yoh.14.26**

**“ Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.”**

**Yoh .15.26**

**“Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia. “**

**Yoh.16.8-11**

**“Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. “.**

**Yoh.16.13 – 14**

**“Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari. “**

Mwombe Roho Mtakatifu akusaidie ktk wokovu kila siku ktk maombi

## 14.UFALME WA MUNGU NI ROHO MTAKATIFU

Ufalme wa mungu ni roho mtakatifu ina maana gani? MUngu huwata wala wote wenye Roho yake kama mfalme wasio na roho yake hupinga mungu kwa matendo na maneno yao,

Roho mtakatifu ni roho ya mungu inayoishi ktk miili ya watu waliokoka kama msaidizi wako hutoa msaada ktk mambo yafuatatayo:

- Kufundisha yote ya Yesu
- Kukumbusha yote ya Yesu
- Kumshuhudia Yesu
- Kukuongoza ktk kweli yaani usitende dhambi
- Kukushauri ushauri wa Yesu ktk unayopitia
- Kukupasha mambo baadaye mambo mapya aliyokuandalia Yesu
- Kukuombea mbele za mungu mahitaji yako
- Kukupa maneno ya kusema mbele ya washtaki wako

**Yoh 14.26** Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.

**Yoh 15.26** Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia.

**Yoh 15.27** Nanyi pia mnashuhudia, kwa kuwa tangu mwanzo mmekuwapo pamoja nami.

**Yoh 16.8**

Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.

**Yoh 16.13**

Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.

# 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church  yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**


Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666

Mwenge DSM Tanzania



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034